



ARUSHA MEAT COMPANY LTD

P.O.BOX 14167

ARUSHA

TANZANIA

TEL: +255272970304

Mob: +255734026767

E-mail: arushameatcompany@yahoo.com

KUMB. NA. AMCL/MTNZ/78/62

DATE: 02/10/2024.

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI. (RE-ADVERTISED)

Arusha Meat Company Limited ni Kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za Makampuni ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inajishughulisha na huduma ya uchinjaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo. Aidha Kampuni hii pia huchakata nyama kwa ajili ya kutengeneza bidhaa mbalimbali. Arusha Meat Company Limited inakaribisha waombaji wenye sifa kujaza nafasi moja (1) iliyowazi kama ifuatavyo:

NB: Tangazo hili limerudiwa kwa mara nyingine tena kutokana na sababu mbalimbali.

1.0 MAUZO NA MASOKO (SALES-PERSONNEL) - NAFASI MOJA (1).

1.1 MAJUKUMU YATAKUWA KAMA IFUATAVYO:

- i. Kufanya mauzo ya bidhaa mbalimbali zinazozalishwa na kuchakatwa na Kampuni kwa wateja kwenye vituo vya mauzo (Sales Point).
- ii. Kuhakikisha anafikia malengo ya siku, mwezi na hatimaye mwaka kwa mauzo kadiri alivyopangiwa.
- iii. Kuhakikisha anatoa huduma bora kwa wateja kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na Kampuni.
- iv. Kuhakikisha anapenya kwenye soko kwa kuuza bidhaa na kuitangaza Kampuni sehemu mbalimbali kadiri iwezekanavyo.
- v. Kufuatilia na kutoa taarifa juu ya shughuli za mauzo kwa msimazi wake.

- vi. Kupokea malalamiko ya wateja katika eneo lake la kazi na kuwasilisha kwa msimamizi wake kwa utekelezaji ili kuweza kudumuisha mahusiano mazuri kati ya mteja na Kampuni.
- vii. Kufuatilia na kutoa taarifa juu ya shughuli za mauzo kwa msimamizi wake.
- viii. Kuhakikisha usafi na mpangilio mzuri kwenye vituo vya mauzo "Sales Point" ili kuweza kuwavutia wateja.
- ix. Kuhakikisha anaweka kumbukumbu sahihi za mauzo ya kila siku kwenye vitabu na mfumo wa mahesabu ya Kampuni.
- x. Kufanya jukumu lingine lolote atakalopangiwa na Mwajiri.

1.2 SIFA ZA MWOMBAJI.

- i) Awe na Astashahada (Certificate in Marketing or Business Administration) ya Masoko na Usimamizi wa Biashara au sifa sawa na hizo kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali.
- ii) Awe na uzoefu katika eneo la mauzo kwa kuitangaza biashara usiopungua miaka miwili (2) na kuendelea.
- iii) Awe na uzoefu wa kutumia "computer".
- iv) Awe na uwezo wa kuongea Kiswahili na Kingereza kwa ufasaha.
- v) Awe na umri kuanzia miaka 18-35.

1.3 MSHAHARA:

Kwa kuzingatia ngazi ya Mishahara ya Arusha Meat Co. Ltd yaani ngazi ya **AMC 2**.

MASHARTI YA JUMLA KWA NAFASI ILIYOTANGAZWA.

- i. Waombaji wawe raia wa Tanzania.
- ii. Waombaji waambatanishe Cheti cha kuzaliwa.
- iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu pamoja na barua iliyoandikwa kwa mkono na kusainiwa.
- iv. Anuani na namba ya simu ya mwombaji na picha moja "Passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.

- v. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, nakala za vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika vyeti vya kitaaluma (professional certificate) kutoka bodi husika na viwe "Certified".
- vi. "Testimonials", "provisional results", "statement of result" hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita **HAVITAKUBALIWA.**
- vii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU, NECTA, NACTE).
- viii. Mwombaji atajigharamia mwenyewe wakati wa usaili.
- ix. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATAPOKELEWA.**
- x. Ajira hii ni ya mkataba wa muda maalum.
- xi. Barua zote zielekezwe kwa;
MENEJA MKUU,
ARUSHA MEAT CO. LTD,
S.L.P 14167,
ARUSHA-TANZANIA.
- xii. Barua zote za maombi zitumwe kwa njia ya Posta au kwa njia ya barua pepe (email) **recruitment@arushameat.co.tz.**
- xiii. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 15/10/2024.

NB: Barua zote zitakazotumwa nje ya utaratibu huu uliolekezwa katika tangazo hili hazitafanyiwa kazi. Aidha kwa wale waombaji ambao walishatuma maombi yao kupitia tangazo la awali hawahitaji kutuma maombi tena.

Tangazo hili limetolewa na: -

MENEJA MKUU
ARUSHA MEAT CO. LTD